

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Dodoma
Anwani ya Simu REGCOM
Simu: 026 2324343/2324384
Nukushi:0262320046/2320121
Barua pepe : ras@dodoma.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P. 914
Dodoma

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Dodoma umepiga marufuku michango holela na isiyo na vibali inayochangishwa kwenye shule za Msingi na Sekondari Mkoani Dodoma kwa kuwa inakwenda kinyume na maelekezo ya Serikali ya awamu ya tano iliyo madarakani.

Marufuku hiyo imetolewa Siku moja baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Jordan Rugimbana kufanya ziara ya kushtukiza kwenye shule ya msingi Chadulu iliyopo Manispaa ya Dodoma na kubaini kuwa Wazazi wa Wanafunzi wanachangishwa fedha kiasi kisichopungua shilingi elfu sita (6000) kwa kila mzazi kwa ajili ya kulipia Deni la ankara ya Maji shuleni hapo, gharama ya mitihani ya majaribio kwa kidato cha nne na saba na fedha kwa ajili ya chakula cha wanafunzi siku watakayopatiwa chanjo; yote hiyo ikichangishwa kinyume cha taratibu na bila kibali cha Serikali.

Kufuatia hali hiyo Mkuu wa Mkoa Rugimbana tayari ameshamwagiza Afisa Elimu wa Mkoa wa Dodoma kutoa waraka maalum kwa Wilaya zote Mkoa wa Dodoma na shule za Umma kukomesha michango hiyo holela isiyo na vibali. Ameongeza kuwa pale ambapo itaonekana kuna sababu za lazima za kuchangisha michango basi taratibu zote za msingi zilizowekwa zifuatwe ikiwa ni kujadiliana pamoja kati ya uongozi wa shule, wilaya na Mkoa na kisha maombi ya kibali yapitie kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya au Manispaa husika, Mkuu wa Wilaya na kisha kutolewa na Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Rugimbana amewasisitiza Maafisa Elimu Mkoa na Wilaya Zote Dodoma kufuatilia shule zilizopo Dodoma kubaini kama zipo ambazo zinaendeleza suala la kuchangisha michango isiyo na vibali maalum vya Serikali na kuwashirikisha Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Wakuu wa Wilaya wote Mkoani Dodoma kukomesha suala hilo la michango holela.

Jeremia Mwakyoma
AFISA HABARI NA MAHUSIANO
OFISI YA MKUU WA MKOA DODOMA
Agosti 25, 2017